# Ahadi za Mungu zenye Uwezo

Robert Dean



Kwa habari zaidi kuhusu Ahadi za Mungu,
msikilize Dk. Dean kwenye
YouTube channel yake,
*Light From The Light*.

# Ahadi za Mungu zenye Uwezo

Dk. Robert L. Dean, Jr.

Haki miliki © 2016 kwa Dean Bible Ministries

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya nyaraka hii inaweza kunakiliwa au kusambazwa kwa namna yeyote au kwa njia yoyote, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodi, au vinginevyo, bila kuidhinishwa kwa kuandikiwa na Robert Dean.

Imechapishwa nchini Marekani.

Maandiko kutoka kwenye Tafsiri ya Biblia Yenye Itifaki

Mungu ametoa mamia ya ahadi za ajabu kwako! Ndiyo, kwako wewe. Biblia sio tu kitabu cha historia ya zamani au matukio yanayohusisha watu wengine; pia ni Neno lake Mungu kwa kila mmoja wetu. Katika kurasa hizo, Mungu ametoa maelfu ya ahadi, nyingi ni kwa ajili yako. Hizi ni ahadi unazoweza kutegemea kila mahali na katika kila hali ya maisha. Mungu ni mwaminifu siku zote; hatalegea wala hatashindwa kamwe kutimiza ahadi zake.

## Ahadi ni nini?

Ahadi ni kiapo cha taadhima, uhakikisho, au dhamana kwamba mtu hakika atafanya kile alichosema atafanya. Thibitisho la hakikisho hili linategemea asili ya yule anayetoa ahadi na uwezo wake wa kutimiza ahadi hizo. Wanadamu hawana uwezo wa kutimiza ahadi wanazozitoa kwa sababu mara nyingi wana tabia zenye upungufu, rasilimali haba, habari isio tosha, au uwezo wa kudhibiti hali ili kutimiza dhamana zao. Ni Mungu pekee ndiye anayeweza kutoa ahadi isio tikisika, isio vunjika, isio na masharti, na isio badilika. Mungu anajua kila kitu na hivyo anajua hali zote zinazozunguka ahadi zake na maisha yako. Hatatoa ahadi asiweze kuitimiza. Yeye ni mwenye nguvu zote, hivyo ana

uwezo wa kutimiza kile anachoahidi. Zaidi ya hayo, yeye ni haki kamilifu; kwa hivyo, kamwe hawezi badilika wala kulikana Neno lake akishalitoa.

> *Kwa kuwa neno la BWANA lina adili, Na kazi yake yote huitenda kwa uaminifu. Huzipenda haki na hukumu, Nchi imejaa fadhili za BWANA.*
> Zaburi 33:4–5

Tunajuaje kwamba Mungu atatimiza Neno lake? Tunajua kwa sababu Mungu ni kweli na kamwe hasemi uongo. (Hesabu 23:19). Alimwahidi Nuhu kwamba atamlinda katika gharika, na alifanya hivyo. Alimwambia Ibrahimu kwamba uzao wake utakuwa utumwani Misri kwa miaka 400, lakini hatimaye atawaokoa na awarudisha katika nchi aliyomwahidi Ibrahimu. Mungu alifanya vivyo hivyo alivyoahidi. Alimwahidi Yoshua ushindi juu ya majeshi yenye nguvu zaidi, na Yoshua akashinda. Aliahidi kumlinda Daudi na kumfanya mfalme. Hata ingawa Sauli alifanya kila aliloliweza kumuua Daudi lakini kamwe hakumuumiza Daudi. Zaidi ya yote, Mungu aliahidi Israeli Masihi, Mwokozi, atakayeokoa dunia kutoka kwenye dhambi. Na Mungu alitimiza



ahadi hiyo pia. Mungu alitimiza ahadi hizi zote na nyingine nyingi.

Baadhi ya mamia, ikiwa si maelfu, ya ahadi katika Biblia zinahusu watu maalum katika hali maalum: ahadi kwa Nuhu au Ibrahimu au Musa. Ahadi zingine zinahusu makundi maalum ya watu na zilitekelezwa nyakati zilizopita. Ahadi nyingi ni dhamana za kudumu zinazojumuisha kanuni za milele ambazo zinaweza kutegemewa siku zote na watu wa Mungu wote katika karne zote. Hizi ndizo ahadi zinazopatikana katika kitabu hiki.

## Ahadi Kuu Zaidi ya Ahadi Zote

Hatuwezi tarajia Mungu atimize ahadi ikiwa hakuitoa hiyo ahadi kwetu sisi. Ahadi ambazo Mungu anatoa kwa mwanadamu ni, isipokuwa moja, ahadi anazotoa kwa wale walio wa familia yake. Lililo la pekee linahusiana na zile ahadi ambazo Mungu anatoa kuhusu njia ya kufanyika mmoja katika familia yake. Kujiunga na familia ya Mungu sio jambo la kuzaliwa kiasili, urithi wa kimbari, ubora wa maadili, usikivu wa kiroho, uhusiano wa madhehebu, au chochote kingine tunachokikamilisha kwa uwezo wetu. Mungu

hatupokei kama wana wake kwa msingi wa talanta, cheo, hadhi ya kijamii, mafanikio, akili, au kuzaliwa. Kuanzia kwa matajiri hadi kwa maskini, kuanzia kwa wenye nguvu na wenye uwezo hadi kwa wanyonge na wadhaifu, wote wanakubalika katika familia ya Mungu kwa njia moja tu. Ahadi dhahiri ya hii inapatikana katika Injili ya nne ya Agano Jipya, Injili ya Yohana.

> *Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;*
>
> Yohana 1:12

Mtume Yohana alipoandika Injili yake, alianza na utangulizi mfupi akiwaambia wasomaji wake kwamba Yesu wa Nazareti kwa hakika alikuwa mungu wa milele ambaye "*alifanyika mwili, akakaa kwetu*" (Yohana 1:14).

> *Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*
>
> Yohana 3:18



Wale wanaompokea ni wale wanaoamini kwamba Yesu ndiye asemavyo ndiye; Mwana wa Mungu ambaye alitoa wokovu wa milele kwa njia ya kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Madhumuni ya Mtu wa Pili wa Utatu wa Mungu, wa milele, mkamilifu, kufanyika mwanadamu ni kwa sababu jamii ya kibinadamu ilikuwa bila msaada kiroho na bila tumaini. Kila mmoja wetu amezaliwa akiwa ametenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Biblia inaelezea hii kuwa kifo hiki cha kiroho. Tunazaliwa tukiwa hai kiasili, lakini tukiwa tumekufa kiroho (Waefeso 2:1).

Hadi leo mara nyingi dhambi haieleweki. Dhambi sio tu kitendo fulani cha kutisha, kisichofikirika; wala haistahili kutambuliwa tu kama tabia au imani isiyokubalika katika jamii. Ingawa hizi zinaweza kuwa dhambi, dhambi inadhuru kwa siri zaidi na ni ngumu kutambuliwa. Maneno yanayotumiwa kueleza dhambi katika lugha asili za Biblia yanamaanisha "kukosa alama au kukosa shabaha." Dhambi ni neno lolote, wazo, au tendo ambalo "linakosa alama" ya tabia kamilifu ya Mungu. Dhambi hutokea wakati mwanadamu anapoasi Muumba wake na kutafuta kuishi bila kumtegemea

Yeye. Ni lazima sote tukiri kwamba tumetenda dhambi, lakini zaidi ya hapo tunapaswa kutambua kwamba tulizaliwa katika hali hii ya dhambi. Sisi sote tulizaliwa tukiwa wenye dhambi.

> *kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*
>
> Warumi 3:23

Kwa kuwa sote tulizaliwa tukiwa tumekufa kiroho, hali hii lazima ibadilishwe. Hatuwezi kufanya chochote kujiokoa kwa sababu ya hali yetu ya kifo cha kiroho. Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hivi. Mabadiliko haya kutoka kwa kifo cha kiroho hadi uzima wa kiroho yanaitwa kuzaliwa upya au "kuzaliwa mara ya pili."

> *si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;*
>
> Tito 3:5

Yesu mwenyewe anaeleza maana ya kuzaliwa mara ya pili katika mazungumzo yake na mtu anayeitwa



Nikodemo. Nikodemo alikuwa Farisayo aliyejulikana sana na pia alikuwa mwalimu wa Biblia wakati wa Yesu. Alisikia kuhusu miujiza ambayo Yesu alifanya na yale ambayo Yesu alifundisha na kujua miujiza hii ilikuwa ishara zilizotabiriwa katika Agano la Kale kuhusu Masihi, Mwokozi aliyeahidiwa na Mungu kwa wanadamu wote. Nikodemo alienda kumwona Yesu ili apate kujua ukweli mwenyewe.

Kama ilivyo mfano ya watu wengi ambao hawana uhakika kabisa waanzie wapi wanapouliza maswali kuhusu mambo ya kiroho, Nikodemo alianza kwa kumwambia Yesu kwamba alitambua kutokana na miujiza Yake kwamba Yesu alitoka kwa Mungu. Kwa hili Yesu alitoa jibu ambalo lilienda hadi kwenye kiini cha jambo hilo.

> *Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*
>
> Yohana 3:3

Yesu alimweleza Nikodemo kwamba mtu huzaliwa mara ya pili kwa kumwamini Yesu, akiwa na imani kuwa Yesu anaweza kumwokoa kutoka katika

dhambi zake. Akitumia jina la Kimasihi la Agano la Kale "Mwana wa Adamu" kujirejelea Mwenyewe, Yesu alisema, "vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa [kusulubiwa], ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele," (Yohana. 3:14–15). Hii ni ahadi ya ajabu ya Mungu ya wokovu. Angetoa suluhisho kwa wanadamu wenye dhambi, linalopatikana kwa wote, lakini lisilotegemea uwezo wa kibinadamu, upendeleo, mamlaka, cheo, au desturi za kidini, bali ni kwa kukubali tu karama ya bure. Tunapokea karama hiyo kwa kuamini kwamba Yesu Kristo alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Mungu hutupatia uzima mpya, uzima wa milele, na kutufanya kuwa hai kiroho kama matokeo ya kumwamini Kristo. Ikiwa hujawahi kumwamini Kristo kama Mwokozi wako, labda huu ndio wakati wako wa kufanya hivyo. Hizi ni baadhi tu ya ahadi ambazo Mungu amekuahidi kuhusu kukupa wokovu.

*Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.*

Luka 19:10



*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Yohana 3:16

*Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.*

Matendo ya Mitume 16:31

*Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.*

Warumi 5:8

*Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*

Mathayo 11:28

*Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini*

*hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?*

Yohana 11:25–26

*Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.*

Yohana 14:6

*Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*

Yohana 20:31

*Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.*

Yohana 3:18

*Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia.*

Yohana 3:36

*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya*



*mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*

Matendo ya Mitume 4:12

*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*

Waefeso 2:8–9

*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,*

Warumi 5:1

*Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima.*

1 Yohana 5:11–12

*wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;*

*ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake, kwa sababu ya kuziachilia katika ustahimili wa MUNGU dhambi zote zilzotangulia kufanywa.*

Warumi 3:24–25

## Ni Kitu Gani Hufanyika Baada ya Wokovu?

Baada ya wokovu, kila mmoja wetu ni kama mzaliwa mpya. Na kama vile mtoto mchanga lazima aanze kukua, vivyo nasi pia. Kukua kiroho inafanana sana na ukuaji wa kimwili. Ni lazima tule lishe yenye afya ili tupate kujijenga kiroho. Ni lazima tujifunze kutembea. Kama vile watoto wachanga wanavyojikwaa na kuanguka wanapojifunza kusimama na kutembea, ndivyo Wakristo pia watajikwaa na kuanguka kiroho, hii ina maana kwamba bado tutatenda dhambi. Tuna maisha mapya ndani ya Kristo, lakini bado tuna asili yetu ile ile ya dhambi na tutaendelea kutenda dhambi nyingi zile zile tulizotenda. Hata hivyo, inatupasa tukumbuke kwamba Yesu Kristo tayari alilipa adhabu ya dhambi hizo pale msalabani. Hii ina



maana hatuwezi kupoteza wokovu wetu. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba kwa kuwa hatukufanya lolote ili kuokolewa, hatuwezi kufanya lolote kupoteza wokovu huo. Ahadi nyingi katika Biblia zinatuhakikishia kwamba tuko salama milele katika wokovu wetu kwa sababu Kristo alilipia dhambi zetu zote msalabani.

## Uhakikisho wa Wokovu

*Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae, na kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu;*

Yuda 1:24

*Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao ni mkuu kuliko wote; wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu.*

Yohana 10:28–29

*Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa*

*wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee.*

Waebrania 7:25

*tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.*

1 Petro 1:4–5

*Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.*

2 Timotheo 1:12

*Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na*



*upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.*

Warumi 8:38–39

*Bwana huzikomboa nafsi za watumishi wake,*
*Wala hawatahukumiwa wote wamkimbiliao.*

Zaburi 34:22

Ingawa tuko salama katika wokovu wetu; walakini, tunapotenda dhambi, ushirika wetu au uhusiano unaoendelea na Mungu huvunjika. Kama vile kutotii kwa mtoto kunavyoathiri uhusiano na mzazi, ndivyo dhambi zetu huzuia uhusiano wetu na Mungu. Hata hivyo, kwa kuwa dhambi hizo zimelipiwa kwa ukamilifu na Kristo Msalabani, msamaha au urejesho unategemea kazi yake aliyoimaliza msalabani. Mungu anasema tu kwamba tunapaswa kukubali makosa yetu kwake, na tunasamehewa papo hapo. Ahadi hii ni mojawapo ya ahadi muhimu zaidi kwa maisha ya Kikristo.

*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*

1 Yohana 1:9

"Kukiri" maana yake ni kukubali au kutambua ya kwamba tumefanya dhambi. Neema ya Mungu ni nyingi sana kwamba Yeye sio tu anasamehe dhambi tunazokubali au kukiri, lakini pia zile ambazo hatukumbuki au hata hatujui ni dhambi.

Tunapokuwa katika ushirika na Mungu Baba; Mungu Roho Mtakatifu ndiye Wakala Mtendaji wa kukua kwetu kwa kiroho akifanya kazi pamoja na Neno la Mungu.

> *Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu;*
>
> 1 Petro 2:2

> *Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*
>
> 2 Petro 3:18

Unapoendelea kujifunza Biblia, utafahamu zaidi na zaidi zile ahadi zenye utukufu ambazo Mungu ametukabidhi. Tunapojifunza ahadi hizi, nazo pia,



zinatumiwa na Mungu Roho Mtakatifu kusaba-bisha ukuaji ndani yetu.

> *Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*
>
> 2 Petro 1:3–4

## Kudai Ahadi za Mungu

Kudai ahadi kunamaanisha kwamba tunamuamini Mungu kwa ahadi ambayo ametuahidi katika Neno Lake. Tunamwamini atalitimiza Neno Lake. Kwa kweli tunasema, "Mungu, uliniahidi hili. Sasa nakuambia ninaamini ahadi yako na nina imani utaitimiza."

Mungu ni mwaminifu na atatimiza ahadi zake daima iwe tunazidai au la. Lakini tunapozidai wakati wa dhiki, basi tunajikumbusha juu ya ahadi za Mungu, kanuni Zake za milele, na uangalifu

alioahidi, nguvu, na mwongozo. Utaratibu huu huanza kwa kuelekeza imani yetu kwenye ahadi maalum ya Mungu.

Imani daima hutazamia kitu fulani. Kumtumaini Mungu si imani katika imani, bali imani katika kauli maalum zilizofunuliwa katika Neno la Mungu. Katika nyakati za shida na maumivu ya moyo, tunatuliza mawazo na hisia zetu kwa kuzingatia Neno la Mungu lisilobadilika na tabia yake isiyobadilika. Hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba ahadi na kanuni hizi zimehifadhiwa katika nafsi zetu, ili tuweze kuzitumia tunapozihitaji.

Hatua ya pili ni kufikiria juu ya ahadi. Hii ndiyo maana ya neno kutafakari katika Biblia: kumakinikia Neno la Mungu na vile mistari hiyo inamaanisha. Ili kufanya hivyo, tunapaswa kusoma ahadi katika muktadha wake wa kimaandiko. Tunapaswa kufikiria juu ya kile ambacho ahadi inasema, kuchunguza hoja na msingi wa ahadi. Mara nyingi ahadi huimarishwa juu ya sifa bainifu ya tabia ya Mungu; upendo Wake, uweza Wake, utakatifu Wake, haki Yake, au uwezo Wake wa kujua yote.

Kwa mfano, ahadi nyingi zinajumuisha tazamio kwamba Mungu amejua kuhusu matatizo yetu



milele hata na milele. Katika uweza Wake, Yeye ni mkuu kuliko kiwewe au kizuizi chochote tunachokabiliana nacho maishani. Kwa njia ya neema yake, ametukirimia mambo yote: kwa hivyo, “Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?” (Warumi 8:31b).

Ahadi moja mahususi inayojulikana kwa wengi ni 1 Petro 5:7 “huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.” Tukiangalia muktadha, tunaweza kufikiria juu ya ahadi. Kuanzia katika 1 Petro 5:5, Petro anaandika, “Vivyo hivyo ninyi vijana watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu mpate kuhudumiana kwa sababu ‘Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.”

Petro anaamuru vijana waelekezwe kwenye mamlaka. Hiki ndicho kiini cha unyenyekevu: kuelekezwa ipasavyo kwa mamlaka ambayo Mungu ameweka juu yako nyumbani, mahali pa kazi, kanisani, “kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.” Kisha mstari wa sita na wa saba unasema, “Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku

mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu." Ahadi hii inatufahamisha jinsi ya kujinyenyekeza. "Kwa kumtwika Yeye fadhaa zetu zote," tunamruhusu atujali. Sababu ya msingi ya ahadi hiyo inakuza wazo la upendo thabiti wa Mungu na utunzaji wake kwa mwamini. Kwa hivyo, tunapaswa kumtwika wasiwasi na mahangaiko yetu kwake; mwachie Mungu ashughulikie hali hiyo kwa wakati wake kisha utulie kuihusu.

Ahadi hii hutumiwa mara kwa mara wakati wa mafadhaiko, masumbuko, wasiwasi, na mahangaiko. Hata hivyo, kifungu hicho kinaendelea kusema katika 1 Petro 5:8, "Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzungukazunguka akitafuta mtu ammeze." Na dhambi kuu ya shetani ilikuwa ipi? Ujeuri.

Alitaka kuchukua mahali pa Mungu na kuabudiwa kama Mungu. Maada ya 1 Petro 5 ni umuhimu wa kuwa chini ya mamlaka ya Mungu, ya kutokuwa na kiburi. Ili kuepuka kujitegemea kwa kiburi, tunaambiwa tumtwike yeye fadhaa zetu kwa sababu anatujali.



Kwa kuelewa undani wa ahadi, tunaweza kukuza mantiki ya msingi ya ahadi, msingi wa mafundisho ya ahadi, ambayo ni upendo wa Mungu kwa kila mmoja wetu kama watoto Wake, wanajumuiya wa familia yake ya kifalme. Kwa sababu Mungu anajali na ana uwezo mkubwa zaidi wa kushughulikia matatizo yetu, tunakata kauli kwamba tunapaswa kuacha kuhangaikia mambo yote maishani. Ikabidhi mikononi mwa Bwana na uiache hapo.

Katika kurasa zifuatazo kuna idadi ya ahadi za Mungu, zimewekwa kulingana na mada, ambazo unaweza kutumia na kuweka katika matendo kwa hali inayofaa.

Unaweza kutumia kikamilifu ahadi hizi ikiwa utaziweka kwenye.

## Umuhimu wa Kujua Ahadi

*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika*

*wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*

2 Petro 1:3–4

## Ulinzi wa Mungu Katika Dhiki

*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.*

Zaburi 46:1

*Bwana atakuwa ngome kwake aliyeonewa,*
*Naam, ngome kwa nyakati za shida.*

Zaburi 9:9

*Nijapokwenda kati ya shida utanihuisha,*
*Utanyosha mkono juu ya hasira ya adui zangu,*
*Na mkono wako wa kuume utaniokoa.*

Zaburi 138:7

*Ee Bwana, nguvu zangu, ngome yangu, na kimbilio langu siku ya taabu, kwako wewe watakuja mataifa yote toka ncha za dunia, wakisema, Baba zenu hawakurithi kitu ila uongo, naam, ubatili na vitu visivyofaa.*

Yeremia 16:19



*Kwa maana mimi, asema Bwana, nitakuwa ukuta wa moto kuuzunguka pande zote, nami nitakuwa huo utukufu ndani yake.*

Zekaria 2:5

*Mungu wa milele ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; Akasema, Angamiza.*

Kumbukumbu la Torati 33:27

*Bwana ni mwema, ni ngome siku ya taabu; naye huwajua hao wamkimbiliao.*

Nahumu 1:7

*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa.*

Wafilipi 4:11–13

*Yeye atakuokoa na mateso sita; Naam, hata katika saba hapana uovu utakaokugusa.*

Ayubu 5:19

*ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.*

1 Wakorintho 2:5

*Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu. Kwa hiyo napendezwa na udhaifu, na ufidhuli, na misiba, na adha, na shida, kwa ajili ya Kristo. Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu.*

2 Wakorintho 12:9–10

*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.*

Wafilipi 4:19



*Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.*

Yakobo 1:2–4

## Masumbuko na Wasiwasi

*huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.*

1 Petro 5:7

*usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usi-fadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.*

Isaya 41:10

*Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja*

*na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*

Wafilipi 4:6–7

*Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.*

Yohana 14:27

*Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike.*

Kumbukumbu la Torati 31:8

*Umtwike Bwana mzigo wako naye atakutegemeza, Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele.*

Zaburi 55:22

*Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika*



*kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.*

Warumi 8:28

*Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi;*

2 Wakorintho 4:8–9

## Tabia ya Mungu

*Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?*

Warumi 8:31b

*Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu; Maana, njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu, asiye na uovu, Yeye ndiye mwenye haki na adili.*

Kumbukumbu la Torati 32:4

*Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele.*

Waebrania 13:8

*shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*

1 Wathesalonike 5:18

*Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute; Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo ame-nena, hatalifikiliza?*

Hesabu 23:19

## Faraja ya Mungu

*Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza.*

Isaya 43:2

*Kwa ajili ya hayo Bwana atangoja, ili awaonee huruma, na kwa ajili ya hayo atatukuzwa, ili awarehemu; kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu; heri wote wamngojao.*

Isaya 30:18

*Ndiwe sitara yangu, utanihifadhi na mateso, Utanizungusha nyimbo za wokovu.*

Zaburi 32:7



*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*

1 Wakorintho 10:13

*Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;*

Waefeso 3:20

*Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.*

1 Petro 4:12–13

*Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja*

*yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu.*

2 Wakorintho 1:3–4

*Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi.*

Mathayo 11:28–30

*Huwaponya waliopondeka moyo, Na kuziganga jeraha zao.*

Zaburi 147:3

*Katika wingi wa mawazo ya moyoni mwangu, Faraja zako zaifurahisha roho yangu.*

Zaburi 94:19

*Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena;*



*kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*

Ufunuo wa Yohana 21:4

## Uaminifu wa Mungu

*Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee, Lakini sijamwona mwenye haki ameachwa Wala mzao wake akiomba chakula.*

Zaburi 37:25

*Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, Kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi; Uaminifu wako ni mkuu.*

Maombolezo 3:22–23

*Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto, hutateketea; wala mwali wa moto hau-takuunguza.*

Isaya 43:2

*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.*

Wafilipi 4:19

*Ee Bwana, neno lako lasimama Imara mbinguni hata milele. Uaminifu wako upo kizazi baada ya kizazi, Umeiweka nchi, nayo inakaa. Kwa hukumu zako vimesimama imara hata leo, Maana vitu vyote ni watumishi wako.*

Zaburi 119:89–91

*Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na kitu.*

Zaburi 23:1

*Kwa kuwa Bwana hupenda haki, Wala hawaachi watauwa wake. Wao hulindwa milele, Bali mzao wa wasio haki ataharibiwa.*

Zaburi 37:28

*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.*

Waebrania 13:5



## Kutegemea Mungu

*Nawe utajifurahisha kwa Bwana, Naye atakupa haja za moyo wako. Umkabidhi Bwana njia yako, Pia umtumaini, naye atafanya.*

Zaburi 37:4–5

*Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.*

Mithali 3:5–6

*Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini. Mtumainini Bwana siku zote Maana Bwana YEHOVA ni mwamba wa milele.*

Isaya 26:3–4

## Hofu

*usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam,*

*nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.*

Isaya 41:10

*Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike.*

Kumbukumbu la Torati 31:8

*Msiogope, simameni tu, mkauone wokovu wa Bwana atakaowafanyia leo; kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele.*

Kutoka 14:13a

*wala msiteteme, wala msiingiwe na hofu kwa ajili ya wao; kwa maana Bwana, Mungu wenu, ndiye awaandamaye kwenda kuwapigania juu ya adui zenu, ili kuwaokoa ninyi.*

Kumbukumbu la Torati 20:3b-4

*Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.*

2 Timotheo 1:7



*Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani?*

Zaburi 27:1

*Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, atanisitiri katika sitara ya hema yake, Na kuniinua juu ya mwamba.*

Zaburi 27:5

*Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara, Maana Wewe, Bwana, peke yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama.*

Zaburi 4:8

*Siku ya hofu yangu nitakutumaini Wewe; Kwa msaada wa MUNGU nitalisifu neno lake. Nimemtumaini Mungu, sitaogopa; Mwenye mwili atanitenda nini?*

Zaburi 56:3–4

*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka*

*milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.*

Zaburi 46:1–3

## Msamaha

*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.*

1 Yohana 1:9

*Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako.*

Isaya 43:25

*Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.*

Zaburi 103:12

*Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.*

Isaya 1:18



*Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.*

Isaya 53:5–6

*Kwa kuwa Bwana hatamtupa mtu Hata milele. Maana ajapomhuzunisha atamrehemu, Kwa kadiri ya wingi wa huruma zake. Maana moyo wake hapendi kuwatesa wanadamu. Wala kuwahuzunisha.*

Maombolezo 3:31–33

*mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi;*

Kutoka 34:7a

*Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*

Waefeso 1:7

## Nguvu ya Maombi

*Kama ningaliwaza maovu moyoni mwangu, Bwana asingesikia.*

Zaburi 66:18

*Na itakuwa ya kwamba, kabla hawajaomba, nitajibu; na wakiwa katika kunena, nitasikia.*

Isaya 65:24

*Maskini huyu aliita, Bwana akasikia, Akamwokoa na taabu zake zote.*

*Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake hukielekea kilio chao.*

*Walilia, naye Bwana akasikia, Akawaponya na taabu zao zote.*

Zaburi 34:6, 15, 17

*ombeni bila kukoma;*

1 Wathesalonike 5:17

*Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.*

Yeremia 33:3



*Bwana yu karibu na wote wamwitao, Wote wamwitao kwa uaminifu.*

Zaburi 145:18

*Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.*

Yohana 16:24

*Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.*

Mathayo 21:22

*Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa.*

Mathayo 7:7–8

*Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

1 Yohana 5:14–15

## Nguvu

*Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo.*

Isaya 40:29

*Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu.*

Yohana 16:33

*kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu.*

Luke 1:37

*Bwana ni mwema, ni ngome siku ya taabu; naye huwajua hao wamkimbiliao.*

Nahumu 1:7

*Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.*

Mithali 3:5–6



*Wewe, Bwana, nguvu zangu, nakupenda sana; Bwana ni jabali langu, na boma langu, na mwokozi wangu, Mungu wangu, mwamba wangu ninayemkimbilia, Ngao yangu, na pembe ya wokovu wangu, na ngome yangu.*

Zaburi 18:1–2

*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.*

Zaburi 46:1–3

*Nafsi yangu imeyeyuka kwa uzito, Unitie nguvu sawasawa na neno lako.*

Zaburi 119:28

## Kumtazamia Bwana

*bali wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai;*

*watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia.*

Isaya 40:31

*Umngoje Bwana, uwe hodari, Upige moyo konde, naam, umngoje Bwana.*

Zaburi 27:14

*Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja, Na neno lake nimelitumainia.*

Zaburi 130:5

*Ukamilifu na unyofu zinihifadhi, Maana nakungoja Wewe.*

Zaburi 25:21

*Kwa kuwa nakungoja Wewe, Bwana, Wewe utajibu, Ee Bwana, Mungu wangu.*

Zaburi 38:15

*Na sasa ninangoja nini, Ee Bwana? Matumaini yangu ni kwako.*

Zaburi 39:7



*Ee Bwana, unijulishe njia zako, Unifundishe mapito yako, Uniongoze katika kweli yako, Na kunifundisha. Maana Wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, Nakungoja Wewe mchana kutwa.*

Zaburi 25:4–5

*(Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona.)*

2 Wakorintho 5:7

## Neno la Mungu

*Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi.*

Zaburi 119:11

*Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

Waebrania 4:12

*Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*

2 Timotheo 3:16–17

*lakini, kama ilivyoandikwa, Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (Wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) Mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.*

1 Wakorintho 2:9

*Mimi ni mgeni katika nchi, Usinifiche maagizo yako.*

Zaburi 119:19

*Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.*

Zaburi 119:105

*Majani yakauka, ua lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele.*

Isaya 40:8



*Maana kwako Wewe iko chemchemi ya uzima, Katika nuru yako tutaona nuru.*

Zaburi 36:9

*Kufafanusha maneno yako kwatia nuru, Na kumfahamisha mjinga.*

Zaburi 119:130

*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*

Yohana 17:17

*Jumla ya neno lako ni kweli, Na kila hukumu ya haki yako ni ya milele.*

Zaburi 119:160

## Majonzi na Hasara

*Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.*

1 Wathesalonike 4:13–14

*Ndugu zangu, nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kurithi kutokuharibika. Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.*

1 Wakorintho 15:50–52

*Ina thamani machoni pa Bwana Mauti ya wacha Mungu wake.*

Zaburi 116:15

## Je, Una Maswali Kuhusu Maisha?

Katika ulimwengu ambao kila kitu kinaonekana kuwa kibaya zaidi siku hadi nyingine, je, unatafuta ukweli na utulivu wa kushikilia? Je, umechoka kusikia kile ambacho Mkristo anapaswa kuwa anafanya bila kupewa namna na jinsi ya kufanya? Au, je, unajiuliza ikiwa hata Mungu yuko, na ikiwa hivyo, jinsi ya kupata majibu ya maswali kumhusu?



Je, ungeshangaa kujua kwamba Biblia kimsingi ni hadithi ya mpango mkamilifu wa Mungu kwa ajili ya wanadamu hapa duniani na katika umilele? Inakuhusu leo kama ilivyokuwa katika siku zile iliandikwa. Katika **www.deanbibleministries.org** utapata majibu kwa maswali magumu ya maisha na kujifunza kuhusu upendo wa ajabu wa Bwana Yesu Kristo kwako. Kwa nini usitembelee leo?

Kwa nyenzo za ziada za
kujifunza Biblia na
Dk. Robert L. Dean, Jr.,
tafadhali tembelea:

www.deanbibleministries.org

www.westhoustonbiblechurch.org



## Kuhusu Mwandishi

**Dkt. Robert L. Dean, Jr.**

Robert Dean, Jr. ni mchungaji wa West Houston Bible Church, Houston, Texas, na Rais wa Dean Bible Ministries (deanbibleministries.org). Dk. Dean amekuwa mchungaji kwa zaidi ya miaka arobaini na amealikwa kuzungumza katika makanisa mengi kote Marekani. Amefundisha katika Vyuo vya Biblia na pia katika Chafer Theological Seminary. Dk. Dean pia amehusika katika huduma mbalimbali za Ulaya Mashariki tangu 1994—Urusi, Belarusi, na Ukraini ambako amefundisha katika Chuo cha Biblia cha Word of God Bible College tangu 2001. Pia amefundisha katika makanisa nchini Zambia na Afrika Kusini. Mafundisho yake na maelfu ya masaa ya mafundisho ya Biblia yanaweza kupatikana kwenye tovuti yake.

Kwa mafunzo zaidi ya Biblia, tembelea:

**www.deanbibleministries.org**

**www.westhoustonbiblechurch.org**